



**USAID**  
KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI



*Lishe Endelevu itasaidia kuboresha hali ya lishe ya wanawake, watoto na vijana katika mikoa minne ya Tanzania.*

## TANZANIA

### LISHE ENDELEVU

Licha ya maendeleo na juhudi za serikali katika kutatua tatizo la lishe duni, utapiamlo bado ni tatizo nchini Tanzania. Serikali ya Tanzania imeonesha jitihada kubwa kwenye masuala ya lishe kupitia mpango mkakati wa uratibu wa lishe kwenye sekta mtambuka wa kitaifa wa shunguli za lishe unaoambatana na sera za sekta mtambuka, mifumo na miundo. Mpango mkakati huo umeithibitishia Serikali ya Tanzania ahadi ya kupunguza tatizo la udumavu kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano (5) kutoka asilimia 34 hadi asilimia 28 ifikapo mwaka 2021.

Kupitia mradi wa Lishe Endelevu, Serikali ya Marekani itachangia lengo hili la taifa kwa:

- Kupunguza udumavu kwa watoto chini ya umri wa miaka 5 katika mikoa minne.
- Kuongeza idadi ya wanawake walio katika umri wa kuzaa kula vyakula vyenye mchanganyiko kwa kiwango kinachokubalika.
- Kuongeza idadi ya watoto wenye umri wa miezi 6-23 kula vyakula vyenye mchanganyiko sahihi na kwa nyakati sahihi.

### MATOKEO YANAYOTARAJIWA

Lishe Endelevu itafikia zaidi ya wanawake milioni 1.5 walio katika umri wa kuzaa, watoto milioni 1.1 walio chini ya umri wa miaka mitano (5), na vijana walio katika rika balehe 330,000 wenye umri wa miaka 15-19 katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Morogoro na Rukwa.

Matokeo yanayotarajiwa ni pamoja na: -

- Kuimarisha uratibu wa sekta mtambuka katika ngazi za halmashauri ili kuboresha hali ya lishe
- Kuboresha afya, lishe, malezi ya watoto, usafi wa mazingira na matumizi ya maji safi na salama
- Kuongeza upatikanaji wa vyakula mbalimbali vilivyo salama, na vyenye lishe bora.

## MADHUMUNI

Lishe Endelevu itasaidia Serikali ya Tanzania kuongeza na kuboresha:

- Uwezo wa mamlaka ya serikali za mitaa kutekeleza mpango mkakati wa Taifa wa sekta mtambuka za lishe katika ngazi ya jamii.
- Vyama vya kiraia na sekta binafsi kuwasiliana na serikali za mitaa ili kuboresha uratibu wa masuala ya lishe ya jamii.
- Upatikanaji na utoaji wa huduma bora za lishe katika vituo vya afya na jamii.
- Uzalishaji na ulaji wa vyakula vyenye virutubishi kwa wingi katika ngazi ya kaya.
- Udhibiti wa usawa wa kijinsia katika mapato na matumizi ya rasilimali za nyumbani ili kuhakikisha upatikanaji wa vyakula mchanganyiko

## SHUGHULI

- Kuwajengea uwezo watendaji wa serikali za mitaa na wahudumu wa afya ili kutekeleza shughuli za lishe kuendana na Mpango mkakati wa kitaifa wa lishe, pamoja na kutengeneza bajeti na mipango ya utoaji wa huduma za lishe, na kuboresha ugawaji na matumizi ya rasilimali.
- Kufanya kazi na Serikali za Mitaa kuhamasisha uwakilishi wa wanawake kwenye kamati na uongozi katika ngazi zote ili kuchagua ajenda ya lishe katika jamii zao.
- Kusaidia mamlaka za Serikali za Mitaa kutambua na kushirikisha wadau wa lishe kutoka asasi za kiraia na sekta binafsi.
- Kuwajengea uwezo watoa huduma za afya kwenye ngazi ya kliniki ili waweze kutoa huduma bora za lishe na ushauri nasaha.
- Kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ngazi ya jamii juu ya mikakati ya mabadiliko ya tabia za kijamii ili kuboresha lishe na matumizi ya maji safi na salama.
- Kufanya kazi na wahudumu wa afya ngazi ya jamii na wakulima wa mfano ili kuwa na shamba darasa kwa uzalishaji bora wa mazao, mifugo wadogowadogo na ufugaji wa samaki na kuhamasisha ulaji wa vyakula vyenye virutubishi kwa wingi.

**BAJETI** Dola za Kimarekani milioni 19.7

### MUDA

Oktoba 2018 – Septemba 2022

### MAENEO YA MRADI

USAID Lishe Endelevu itaboresha hali ya lishe ya wanawake, watoto na vijana balehe katika mikoa minne:

- Dodoma (Halmashauri 6)
- Morogoro (Halmashauri 9)
- Iringa (Halmashauri 3)
- Rukwa (Halmashauri 4)

### WABIA WA UTEKELEZAJI

- Save the Children International (Kiongozi)
- Deloitte
- The Partnership for Nutrition in Tanzania (PANITA)
- Africa Academy for Public Health (AAPH)
- Manoff group

### MAWASILIANO YA USAID

Janeth Said

Afisa Mkatiba Mwakilishi

[JSaid@usaid.gov](mailto:JSaid@usaid.gov)

+255 755 355 393

### MAWASILIANO YA MBIA

Dr. Joyceline Kaganda

Mkuu wa Mradi

[Joyceline.Kaganda@savethechildren.org](mailto:Joyceline.Kaganda@savethechildren.org)

+255 784 729 181

### KWA TAARIFA ZAIDI

Tovuti: [www.usaid.gov/tanzania](http://www.usaid.gov/tanzania)

Facebook: USAIDTanzania

Twitter: @USAIDTanzania